

Atlas: Tupo Tayari kwa Biashara Kutumia Programu ya Rununu!

Kipengele muhimu cha Mpango wa Kuandaa Biashara

Mbinu ya ubunifu kwa uandalizi wa biashara ndogondogo

Zaidi ya miaka 3 iliyopita, Kituo cha Kimataifa cha Maandalizi ya Maafa (GDPC) cha IFRC kimeanzisha na kuzindua programu ya simu inayoshirikisha na kutoa huduma nzuri, Atlas: Tupo Tayari kwa Biashara, ina lengo la kusaidia biashara ndogondogo kuwa na uwezo wa kujiandaa na kuchukua tahadhali. Biashara ndogondogo zina jukumu muhimu katika jamii na masoko ya kimataifa, na kuchangia katika ajira na ugavi. Ni muhimu katika kuchochea na kurejesha shughuli za kiuchumi katika ngazi ya jamii baada ya maafa.

Ingawa wafanyabiashara wadogo wadogo walio wengi wanajua umuhimu wa kujiandaa kwa maafa yanavyoweza kuathiri shughuli zao, tafiti zimeonyesha kwamba idadi kubwa ya wafanyabiashara wadogo wadogo hawajitayarishi kikamilifu. Hii ni kutokana na gharama kubwa ya kifedha na ukosefu wa mwongozo unaoweza kutekelezwa na mara nyingi huweza kusababisha matatizo sio tu kwa biashara, lakini pia kwa jamii zinazoizunguka.


Atlas hupunguza vikwazo hivi kwa kuwa chombo kinachoweza kupatikana ambacho ni bure kwa wafanyabiashara wa ndani, ili kuwasaidia katika kila hatua. Iliundwa mahususi kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo, wamiliki wa biashara au mameneja waweze kujifunza ili kuboresha ujitayarishaji wao kwa kasi yao wenyewe ili waweze kukamilisha kazi peke yao au pamoja na wafanyakazi wao na wanaagizwa kuchunguza utayarishaji wao wa kazi, mitandao na mahusiano, uongozi na utamaduni, mabadiliko ya utayari, na uwezo wa kuwasaidia watu wao katika kazi. Kulingana na maendeleo ya mtumiaji kupitia viwango vya programu nne na majibu yao kwa maswali ya kujiandaa, Atlas kwa uhodari huzalisha 'Mpango wa Urejeshaji miundombinu wakati wa Maafa' ambao huweza kutumiwa sio tu wakati wa maafa, bali pia kufanya utayarishaji na kuelimisha wafanyakazi.

Programu ya simu ya mkononi hutumia vipengele vya maingiliano, ikiwa ni pamoja na vikao vya mazungumzo na Atlas ambayo humwezesha mtumiaji kujua kiwango chake cha kutayarisha, kupima maendeleo yao, na kumuongoza mtumiaji kwenye safari ya kipekee kuleta ujasiri. Njia hii ya kipekee inafanikishwa kupitia mfumo wa usimamizi wa maudhui ya Atlas ambayo yanaweza kubadilishwa ili kuonyesha maudhui ya mahali fulani ya mtumiaji, kutafsiriwa kwa lugha nyingi na lafudhi za eneo fulani, na kubadilishwa ili kuingiza maudhui maalum ya sekta ili kusaidia zaidi biashara na kuwashirikisha.



Atlas: Tupo Tayari kwa Biashara inapatikana katika lugha 7 - Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kiindonesia, Kihispaniola, Kiswahili, na Kivietinamu - na lugha zingine bado zinaendelea kutafsiriwa

Pakua kwenye: preparecenter.org/atlasapp



"Moja kwa moja ni wazi kwamba [Atlas] ilikuwa inahusu urejesho wa hali ya awali na ujasiri wa biashara baada ya maafa, ili kuhakikisha una kila kitu kinachohitajika." - Mmiliki wa biashara ndogo, New Zealand

Ikiwa ni sehemu ya ushirikiano wa mtandao wa Kidunia wa Msalaba, Kituo cha Kuandaa Maafa Duniani (GDPC) ni kituo cha rasilimali ambacho kinasisitiza ubunifu katika utayarishaji wa maafa na inasaidia kugawana na kujifunza maarifa kati ya watayarishaji wa maafa duniani kote. Kipengele kimoja muhimu cha kazi ya GDPC ni kukuza mbinu za ubunifu za utayarishaji wa maafa, kama vile ubunifu wa kutumia teknolojia. Kupitia Mpango wa Kuandaa Biashara, mashirika ya Msalaba Mwekundu na mashirika mengine yanaweza kuwapatia Atlas: Tupo Tayari kwa Biashara katika jamii ili kuimarisha urejesho wa hali ya awali kwa jamii na kupunguza madhara ya maafa.



www.preparecenter.org



gdpc@redcross.org



disaster.preparedness.center



[PrepareCenter](https://PrepareCenter.org)

